



**MINISTÈRE
DE L'EUROPE
ET DES AFFAIRES
ÉTRANGÈRES**

*Liberté
Égalité
Fraternité*

DIRECTION GÉNÉRALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Bureau des concours et examens professionnels

**CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE
SECRETARE DES AFFAIRES ETRANGÈRES
(CADRE D'ORIENT)
AU TITRE DE L'ANNÉE 2024**

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Jeudi 21 septembre 2023

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures

Coefficient : 2

Toute note globale inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire

Dictionnaire autorisé

Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points

COMPOSITION EN SWAHILI

*Composition en swahili à partir d'une question,
rédigée dans cette même langue, liée à l'actualité
(350 mots avec une tolérance de plus ou moins 10%)*

SUJET :

Shirika la Umoja wa Mataifa lina uwezo gani kurejesha amani Afrika ?

**CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE
SECRÉTAIRE DES AFFAIRES ÉTRANGÈRES
(CADRE D'ORIENT)
AU TITRE DE L'ANNÉE 2024**

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Jeudi 21 septembre 2023

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures

Coefficient : 2

Toute note globale inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire

Dictionnaire autorisé

Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points



TRADUCTION EN FRANÇAIS

Traduction en français d'un texte rédigé en swahili

TEXTE AU VERSO

Senegal: 'Ousmane Sonko yuko katika afya njema, lakini ameathirika'

Na mwandishi wetu maalum huko Dakar, David Baché

Mnamo Mei 28, kikosi cha maafisa polisi nchini Senegal walimchukua kiongozi wa upinzani nchini humo Ousmane Sonko kwa nguvu hadi nyumbani kwake huko Dakar, ambapo anashikiliwa tangu wakati huo.

Vikosi vya usalama vya Senegal vinamzuia kuondoka nyumbani kwake, ambako hata mawakili wake hawajaruhusiwa kuingia. Lakini mfanyabiashara wa Senegal Pierre Goudiaby Atepa, mbunifu mashuhuri na mkuu wa kundi la Wawekezaji nchini Senegal, aliweza kubahatika kutokana na idhini ya kipekee kutoka kwa mamlaka kukutana na Ousmane Sonko. Katika mahojiano maalumu na RFI, Pierre Goudiaby Atepa ambaye anataka kuchukua nafasi ya mpatanishi kati ya Rais Macky Sall na Ousmane Sonko ametoa taarifa za kwanza kwa zaidi ya wiki mbili kuhusu Ousmane Sonko, kuhusu hali afya yake na jinsi anavyoendelea akiwa kizuizini cha nyumbani.

Mahojiano hayo yamechukua muda wa saa moja hadi mbili, nyumbani kwa Ousmane Sonko, katika wilaya ya Cité Keur Gorgui, akiwa amezingirwa na polisi. Pierre Goudiaby Atepa, mbunifu mashuhuri wa Senegal, aliweza kwenda nyumbani kwake hivi karibuni.

"Nakuthibitishia, niliweza kumuona nyumbani kwake, niliweza kupata idhini ya kipekee ya kwenda kumuona na tukazungumza. Anaendelea vizuri kiafya. Hata hivyo anaguswa na kila kitu kinachoendelea nchini, kwa kuwa ana wafuasi wengi waliokamatwa, vijana wengi wamekamatwa. Ni wasiwasi mkubwa. Lakini yuko katika afya njema."

Pierre Goudiaby Atepa ni mfuasi mkubwa wa kisiasa wa Ousmane Sonko, lakini pia anadai kuwa na urafiki na Macky Sall. Ndiyo maana anajiona kama mpatanishi, lakini bila kupewa mamlaka. Siku ya Alhamisi wiki iliyopita, baada ya kukutana na mpinzani huyo, mfanyabiashara huyo alitaka kufikisha ujumbe kwa rais.

"Ni mpango wa kibinafsi. Bwana Sonko hakuniomba niende kumuona rais ili nimwambie. Huu ni ujumbe ambao niliuelewa kutokana na mahojiano tuliyokuwa nayo, ya amani, ya maelewano kati ya Wasenegali."

Hakuna ofa maalum ya kisiasa iliyotolewa na Ousmane Sonko. Kufikia sasa, Macky Sall amekataa kuzungumza na Pierre Goudiaby Atepa, ambaye anatumai siku itafika kukutana naye kwa mazungumzo. Ni pamoja na mashirika ya waajiri ambapo anajaribu kupatanisha misimamo ya pande hizo mbili.